

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 30 OCTOBA, 2021
KWENYE UKUMBI WA MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA KILWA.**

MAHUDHURIO.

NA.	JINA	CHEO
1.	GRACE MWAMBE	MWENYEKITI WA BODI
2.	NEGWAKO MWAMBOPE	KATIBU WA BODI
3.	SYLVESTER KALAGILA	MJUMBE
4.	JUMA J. AHMADI	MJUMBE

WAALIKWA.

- | | | |
|----|-------------------|----------|
| 1. | Eng. SAIDI PONGWA | MWALIKWA |
| 2. | Dr. MAHELA NJILE | MWALIKWA |

SEKRETARIET

1. ABDALLAH MCHWEMBO

MWANDISHI WA VIKAO

1. JULIUS MAYEGA

AGENDA ZA KIKAO

1/2021. KUFUNGUA KIKAO

Katibu aliwakaribisha wajumbe katika kikao na kuwaeleza kuwa hiki ni kikao cha kawaida cha Bodi kwa ajili ya kujadili maswala mbalimbali ya manunuzi, baada ya hapo kattibu alimkaribisha mwenyekiti kwa ajili ya kufungua kikao. Mwenyekiti bila kupoteza wakati alikifungua kikao mnamo saa mbili na robo asubui (2:15) asubuhi.

2/2021. KUTHIBITISHA AGENDA.

Jumla ya agenda tano ziliwasilishwa kikaoni ambazo ni;

- I. Kufungua Kikao
- II. Kuthibitisha Agenda
- III. Yatokanayo na Kikao kilichpita cha tarehe 29.9.2021
- IV. Matumizi ya 2,060,000,000/= Kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya uviko 74 ya sekondari na Vituo shikizi 29 kwa njia ya force account.

V. Kufunga kikao.

**3/2021. KUSOMA NA KUTHIBITISHA MHTASARI WA KIKAO CHA BODI
KILICHOFANYIKA TAREHE 29 SEPTEMBER 2021.**

Muhtasari wa kikao cha bodi kilichofanyika tarehe 29. SEPTEMBER 2021 uliwasilishwa, Wajumbe waliupokea muhtasari huo, waliupitia ukurasa kwa ukurasa na ukawekwa saina na Mwenyekiti na Katibu kuwa kumbukumbu halali ya halmashauri.

**4/2021. YATOKANAYO NA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE
29. SEPTEMBER, 2021.**

Yatokanayo na kikao cha bodi ya zabuni kilichofanyika tarehe 29 September 2021. Hakuna yatokanayo yaliyowasilishwa

**5/2021. MAOMBI YA FEDHA KIASI CHA SHILINGI 2,060,000,000/= KWA AJILI YA
UJENZI WA MADARASA YA UVIKO, MADARASA 74 YA SEKONDARI NA 29 YA
VITUO SHIKIZI KWA NJIA YA FORCE ACCOUNT.**

Katibu alitoa ufafanuzi wa matumizi ya fedha kiasi cha shilingi 2,060,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 74 ya sekondari na madarasa 29 ya vituo shikizi. Aidha alitoa mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo kuwa kiasi cha shilingi 1,480,000,000/= zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 74 ya sekondari na shilingi 580,000,000/= zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya vituo shikizi ndani ya wilaya yetu.

Wajumbe walipokea maombi ya fedha hizo pamoja na mchanganuo wake, aidha wajumbe walijadili kwa kina nakuridhia matumizi hayo. Pia walisisitiza kuwa fedha hizo zitumike kwa shughuli zilizopangwa tu na si vinginevyo, pia zisimamiwe kikamilifu kwa ajili ya manufaa ya halmashauri ya kilwa na Taifa kwa ujumla.

6/2021, KUFUNGA KIKAO

Katibu aliwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria na kushiriki vyema kwenye agenda zilizo wasilishwa kikaoni. Baada ya hapo alimkaribisha mwenyekiti. Nae mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa nne na nusu (10:30) asubuhi.

Saini ya Mwenyekiti.....

Saini ya Katibu.....

Tarehe 29/11/2021.....